

TANGAZO



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



Katibu Mtendaji, Baraza la Mitihani la Tanzania anawajulisha watu wote wanaotarajia kufanya Mtihani wa **Kidato cha Nne** (CSEE) na Upimaji wa **Kidato cha Pili** (FTNA) **Novemba, 2024** kama Watahiniwa wa Kujitegemea kwamba;

1. Kipindi cha usajili kitaanza tarehe **01/01/2024** kwa ada ya Shilingi **50,000/=** kwa wanaojisajili **CSEE** na Shilingi **10,000/=** kwa wanaojisajili **FTNA** na kitaishia tarehe **29/02/2024**. Aidha, watakaojisajili kwa **kuchelewa** kuanzia tarehe **01/03/2024** hadi tarehe **31/03/2024** watalipa Shilingi **65,000/=** kwa Watahiniwa wa Kidato cha Nne (**CSEE**) na Shilingi **15,000/=** kwa Watahiniwa wa Upimaji wa Kidato cha Pili (**FTNA**) ikiwa ni ada ya kawaida pamoja na faini.
2. Mtahiniwa atakaye jisajili kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne (**CSEE**) **2024** ni yule ambaye anarudia Mtihani wa **Kidato cha Nne** (CSEE) **au** amefanya na kufaulu **Mtihani wa Maarifa** (QT) katika kipindi kisichozidi Miaka **Kumi** (10) iliyopita **au** amefanya na kufaulu Upimaji wa **Kidato cha Pili** (FTNA) katika kipindi kisichozidi Miaka Kumi (10) iliyopita **au** mwenye sifa zinazolingana na hizo alizopata kutoka nje ya Nchi na kufanyiwa ulinganifu na Baraza la Mitihani la Tanzania.
3. Mtahiniwa atakaye jisajili kufanya Upimaji wa Kidato cha Pili (FTNA) ni yule ambaye anatafuta sifa ya kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne kama Mtahiniwa wa Kujitegemea.
4. Usajili unafanyika kwa njia ya mtandao, kwa kufuata hatua zifuatazo;
 - (a) Fika Kituo unachotarajia kufanya Mtihani ili kupata maelekezo kutoka kwa Mkuu wa Kituo kuhusu usajili wa watahiniwa wa Kujitegemea .
 - (b) Mkuu wa Kituo cha Watahiniwa wa Kujitegemea ataingiza namba rejea ya Mtahiniwa kwenye mfumo wa usajili ili kupata 'Control Number' ya kufanya malipo ya ada ya Mtihani.
 - (c) Mkuu wa Kituo cha Watahiniwa wa Kujitegemea atakukabidhi 'Control Number' ili ukafanye malipo Benki. Mtahiniwa utafanya malipo ya ada ya Mtihani Benki kwa kutumia 'Control Number' uliyo kabidhiwa. Baraza la

Mitihani hufanya na kupokea malipo kupitia Benki ya NMB, CRDB au NBC.

- (d) Fika tena kwa Mkuu wa Kituo cha Watahiniwa wa Kujitegemea ili kusajiliwa kwa ajili ya Mtihani unaotarajia kuufanya. Njoo na vielelezo vyote vinavyohitajika kwenye usajili ambavyo ni pamoja na **picha, orodha ya masomo ya kusajiliwa, Kivuli cha cheti cha Kuzaliwa, namba ya simu na taarifa nyinginezo** zilizo muhimu kusajiliwa.
 - (e) Baada ya usajili kukamilika utapewa nakala **moja** ya fomu ili itunzwe na wewe mwenyewe kwa ajili ya kumbukumbu. Nakala ya **pili** ya fomu, itabaki Kituoni ambapo nakala ya **tatu** ya fomu italetwa Baraza la Mitihani.
5. Ufafanuzi kuhusu utaratibu wa hatua za kufuata katika usajili, umetolewa katika www.necta.go.tz. Waombaji wote **wanasisitizwa** kuhakikisha wanajiliwa mapema kwani mfumo wa usajili utafungwa baada ya kipindi cha usajili kumalizika.

Imetolewa na;

KATIBU MTENDAJI